# CLASS 6 END TERM 3 DECEMBER 2021

# KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1-15, kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo chini. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Hakuna jambo lolote ____**1**____ gumu duniani. Ugumu na ____**2**____ wa jambo ____**3**____ tu katika akili zetu, ukiamini kuwa jambo ni gumu, basi ujue kuwa ____**4**____. Jambo lijapokuwa gumu namna ____**5**____; na uamini kuwa litawezekana, ____**6**____ litawezekana. Hivyo basi kufaulu na kushindwa kwetu katika jambo kunaanzia akilini ____**7**____. Mawazo chanya hutufanya tufaulu; bali mawazo ____**8**____ hutufanya tufeli ____**9**____ tukose kufaulu.

Bingwa wa marathoni ____**10**____, Eliud kipchoge, aliamini kuwa hakuna binadamu aliyekuwa na mpaka ____**11**____ kutenda jambo lolote. ____**12**____ imani hiyo si ya kukubaliwa na watu wote, lakini ____**13**____ kuwa binadamu wa ____**14**____ kukimbia mbio za marathoni chini ya saa mbili. ____**15**____ palipo na nia pana njia.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** lilio | **B.** ambalo | **C.** lililo | **D.** ambayo |
| **2.** | **A.** ubaya | **B.** urahisi | **C.** uraisi | **D.** uzuri |
| **3.** | **A.** umo | **B.** iko | **C.** uko | **D.** una |
| **4.** | **A.** utaliweza | **B.** umeliweza | **C.** huliwezi | **D.** hutaliweza |
| **5.** | **A.** ipi | **B.** gani | **C.** aje | **D.** vipi |
| **6.** | **A.** na | **B.** pia | **C.** basi | **D.** ndio |
| **7.** | **A.** yetu | **B.** petu | **C.** zetu | **D.** mwetu |
| **8.** | **A.** hasi | **B.** mabaya | **C.** mepesi | **D.** mazuri |
| **9.** | **A.** wala | **B.** ama | **C.** bali | **D.** ila |
| **10.** | **A.** barani | **B.** nchini | **C.** duniani | **D.** Africa |
| **11.** | **A.** la | **B.** ya | **C.** za | **D.** wa |
| **12.** | **A.** Ingawa | **B.** Kama | **C.** Isipokuwa | **D.** Lakini |
| **13.** | **A.** ilimwezesha | **B.** itamwezesha | **C.** iwazesha | **D.** humwezesha |
| **14.** | **A.** mbele | **B.** mwisho | **C.** kwanza | **D.** awali |
| **15.** | **A.** kwani | **B.** kweli | **C.** ndio | **D.** basi |

**Kutoka swali la 16-30 jibu kulingana na maagizo.**

16. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.**
**Unyasi umenyauka wenyewe**
A. Unyasi yamenyauka yenyewe
B. Manyasi zimenyauka zenyewe
C. Manyasi yamenyauka yenyewe
D. Nyasi zimenyauka zenyewe

17. Ni kitenzi gani kiko katika kauli ya kutendewa?
A. Pigwa B. Chelewa
C. Lipiwa D. Jeruhiwa

18. Mtoto wangu ameumia vibaya.
Maneno yaliyopigiwa mstari mtawalia ni
A. kielezi, kivumishi B. kitenzi, kielezi
C. nomino, kivumishi D. kivumishi, kielezi

19. Ni sentensi ipi iliyo sahihi kisarufi?
A. Kabati langu limevunjika
B. Mtoto huyu ni msafi
C. Ari yake ni mpya
D. Kifagio kile ni changu

20. Kanusha sentensi ifuatayo
**Bakari alicheza mpira vizuri**
A. Bakari hachezi mpira vizuri
B. Bakari hakucheza mpira vizuri
C. Bakari hatacheza mpira vizuri
D. Bakari alicheza mpira vibaya

21. Ni neno lipi liko katika ngeli ya U-U?
A. Ukuta B. Uta
C. Ugali D. Uzi

22. Kamilisha kwa neno sahihi
Likizo hii tutaenda mashambani________.
A. yote B. wote
C. zote D. sote

23. Kamilisha sentensi kwa kirejeshi 'ndi' sahihi.
Je, wewe_____uliyechora picha hii?
A. ndiye B. ndiwe
C. ndio D. ndie

24. Ni sentensi gani imetumia 'ki' ya masharti?
A. Mvua ikinyesha tutapanda
B. Walikuwa wakila nilipoingia
C. Kijiji chetu kimeendelea
D. Mtu yule anatembea kijeshi

25. **Geuza katika usemi taarifa; "Chakula kitapikwa," mama alisema.**
A. Mama alisema kuwa chakula kilipikwa.
B. Mama alisema kuwa chakula kimepikwa
C. Mama alisema kuwa chakula kingepikwa
D. Mama alisema kuwa chakula kitapikwa

26. Ni nomino gani isiyotokana na kitenzi tibu?
A. Tabibu B. Tabu
C. Tiba D. Utabibu

27. Ni neno gani kati ya haya si kitawe?
A. Zaa B. Paa C. Kaa D. Baa

28. Mstari mmoja katika ubeti huitwa______
A. mizani B. kibwagizo
C. kiwa D. mshororo

29. Ni kiumbe gani kimelinganishwa sawa na kikembe chake?
A. Simba - kisui
B. Bata - kinda
C. Ndege - kifaranga
D. Chura - kiluwiluwi

30. **Kamilisha methali ifuatayo:**
**Asiyekujua**
A. hakutambui B. hakudhamini
C. hakuthamini D. hakufahamu

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.**

Je, unajua ugonjwa ambao umekuwa ukiua watu wengi zaidi barani Afrika? Pengine jibu lako laweza kuwa ni saratani, Ukimwi ama korona. Ukweli ni kuwa magonjwa matatu niliyotaja ni hatari kwa binadam lakini si jawabu la swali langu. Ugonjwa wa saratani ni hatari kwa sababu hauna tiba na haujulikani chanzo chake. Wanasayansi wamekuwa wakifanya utafiti lakini kufikia sasa hawajagundua chanzo wala dawa ya kuzuia ugonjwa huu yaani raksini. Mgonjwa anaweza kunusurika kutokana na ugonjwa huu iwapo utagunduliwa mapema na kushughulikiwa.

Ugonjwa wa Ukimwi ulianza miaka ya elfu moja mia tisa na themanini. Chanzo chake (yaani mahali ulikotoka) hakijulikani. Lakini unasababishwa na virusi vya HIV vinavyosababishwa na ukosefu wa kinga katika mwili wa binadamu. Hii ndiyo sababu ugonjwa wenyewe unaitwa Ukimwi hauna tiba, kuna dawa zinazoweza kuzuia makali yake na kumwongezea mgonjwa maisha anapoendelea kuzitumia.

Ugonjwa wa korona umeua maelfu ya watu kwa muda mfupi tangu uanze. Ugonjwa huu ulianza mwaka wa elfu mbili na kumi na tisa. Inadhaniwa kuwa ulianza Uchina ingawa hayajathibitishwa. Ugonjwa huu husababishwa na virusi vya Covid 19'. Wanasayansi wameshafanya utafiti na kugundua dawa ya kuzuia ugonjwa huu kufikia sasa mamilioni ya watu ulimwenguni kote wameshapata chanjo ya kuzuia ugonjwa huu.

Ugonjwa hatari zaidi ambao kwa miaka mingi umekuwa ukiwaua watu wengi sana barani Afrika ni malaria. Watu wengi huenda wasiamini hilo lakini huo ndio ukweli na ndilo jawabu la swali langu. Malaria ni ugonjwa hatari sana kwa sababu unaua. Ugonjwa huu husababishwa na vimelea vinavyotokana na mbu jike aina ya anofelesi. Vimelea hivi huharibu chembechembe nyekundu za damu na kusababisha ukosefu wa damu mwilini.

Kwa muda mrefu ugonjwa wa malaria umekuwa tishio kwa afya ya watu wa bara hili ilhali kwa watoto walio chini ya miaka mitano. Juhudi nyingi zimefanywa kukabiliana na ugonjwa huu bila mafanikio makubwa. Ingawa kumekuwa na dawa za kuponya, zimekuwa hazijafua dafu kuzuia athari za ugonjwa huu. Mbinu za kuzuia malaria kama vile kufyeka nyasi kunyunyizia maji yaliyotulia mafuta, kulala ndani ya neti na nyinginezo zimetumika bila mafanikio ya maana.

Hata hivyo mwaka huu umekuwa mwaka wa habari njema za mafanikio. Kwani baada ya miaka thelathini ya utafiti, hatimaye dawa ya kuzuia malaria imepatikana. Majaribio tayari yameshafanywa na kuonyesha kuwa dawa hii inafanya kazi. Hivi karibuni ugonjwa wa malaria hautakuwa tishio tena. Heko na pongezi ziwaendee wanasayansi wetu.

**31.** Kati ya magonjwa matatu yaliyotajwa katika aya ya kwanza ni upi unaoua watu wengi zaidi barani Afrika?
A. Saratani B. Hakuna
C. Ukimwi D. Korona

**32.** Ni kauli gani kweli kuhusu ugonjwa wa saratani?
A. Unaweza kuzuiwa unapogunduliwa mapema
B. Unajulikana chanzo chake
C. Una dawa yaani raksini
D. Si hatari

**33.** Ni kauli gani si kweli kuhusu Ukimwi?
A. Ni ukosefu wa kinga mwilini
B. Unasababishwa na virusi
C. Una tiba.
D. Una dawa za kuzuia makali yake.

**34.** Ugonjwa wa korona ulianza mwaka wa
A. 2016 B. 2019 C. 1919 D. 1970

**35.** Inadhaniwa kuwa ugonjwa wa korona ulianza
A. Uchina B. Marekani C. Urusi D. Italia

**36.** Sifa inayoufanya ugonjwa wa malaria kuwa hatari ni kuwa
A. unaambukizika
B. unaenea haraka
C. unasababishwa na mbu
D. unaua

**37.** Ugonjwa wa malaria umekuwa tishio kwa afya ya watoto_______
A. walio chini ya miaka mitatu
B. waliozidi miaka mitano
C. walio chini ya miaka mitano
D. walio tumboni mwa mama

**38.** Ni gani kati ya hizi si mbinu ya kuzuia malaria?
A. Kuchemsha maji
B. Kufyeka nyasi
C. Kunyunyizia maji mafuta
D. Kulala ndani ya neti

**39.** Mwaka huu umekuwa wa habari njema za mafanikio kwa kuwa___________
A. dawa ya kuangamiza mbu imepatikana
B. dawa ya kuzuia malaria imepatikana
C. dawa ya kuponya malaria imepatikana
D. dawa ya kupunguza makali ya malaria imepatikana

**40.** Utafiti wa kutafuta dawa yenyewe ulifanywa kwa muda wa
A. siku thelathini
B. miezi thelathini
C. wiki thelathini
D. miaka thelathini

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.***

Baada ya safari zake katika sehemu mbali mbali za nchi kikazi, Bi Aseyo alirejea tena mjini Nairobi. Nairobi ndiko kulikokua na ofisi yake ambako alipoingia,mipango yake ya kazi lakini shughuli zenyewe zilifanyika mahali popote wateja wake walikomhitaji.

Bi Aseyo ni mpishi hodari. Ujuzi wake wa kupika vyakula mbalimbali umemletea sifa tele. Anajua kupika kila aina ya chakula. Chakula chake chaweza kuliwa na mtu mwenye hadhi yoyote. Kila anayekula chakula chake haachi kukisifu jinsi kilivyo kitamu. Watu hutaka kujua viungo anavyotumia kukifanya chakula kuonja utamu jinsi hiyo. Ajabu ni kuwa yeye hutumia tu viungo vya kawaida. Kutokana na majibu yake, watu hutambua kuwa ana kipawa cha upishi. Mtu mwenye kipawa cha upishi anaweza kutumia viungo vya kawaida lakini chakula kikawa na utamu wa kipekee.

Bi Aseyo si mpishi wa chakula tu, yeye pia ni mwokaji hodari. Yeye huoka mikate na hata keki, keki zake huwa ni tamu ajabu. Kila anayezionja hutaka kuonja tena na tena, kweli mchovya asali hachovyi mara moja.

Kutokana na uhodari wake wa upishi, watu wengi humwita katika sherehe ili awapikie ama awaokee keki. Hivyo basi utampata katika harusi, sherehe za kuzaliwa, mahafali n.k.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Siku moja Bi Aseyo aliporejea Nairobi kutoka katika shughuli zake sehemu mbalimbali,alijihisi mnyonge. Yeye alidhani kuwa ulikuwa ni uchovu wa kawaida uliosababishwa na shughuli za kazi. Aliendà kwenye duka la dawa na kununua dawa za maumivu. Alimeza dawa hizo lakini uchovu haukuisha. Ilibidi aende akamwone daktari. Daktari alimwuliza iwapo alikuwa amesafiri. Alishangaa ni vipi usafiri ulihusiana na ugonjwa wake. Hata hivyo alikubali kuwa alikula amesafiri sehemu mbalimbali za nchi. Daktari alimshauri aende kwenye maabara ili apimwe damu.

Baada ya matokeo kutokea ilibainika kuwa alikuwa na malaria nyingi mwilini na kuwa alihitaji kulazwa lakini madaktari walisema kuwa kiwango cha malaria ilikuwa juu; na kuwa kinaweza kuhatarisha maisha yake iwapo hangeshughulikiwa vizuri. Wauguzi walimwongoza hadi kwenye wodi na kumweka dawa kupitia kwenye mikono kwa njia ya mrija. Baada ya siku tatu walipata ruhusa ya kurudi nyumbani. Lakini kabla ya kuondoka madaktari walimwelimisha kuhusu hatari za malaria. Walimweleza kuwa alifanya jambo la busara kutafuta matibabu mapema. Kwa kweli ni vizuri kujihadhari kabla ya hatari aliwashukuru madaktari.

---

**41.** Safari za Bi.Aseyo katika sehemu mbalimbali za nchi zilikuwa za
A. kitalii
B. kikazi
C. kielimu
D. kibiashara

**42.** Ni kitu gani kilichomletea Bi Aseyo sifa tele?
A. Usafiri wake sehemu mbalimbali za nchi
B. Ujuzi wake wa kupanga mipango ya kazi
C. Shughuli zake jijini Nairobi
D. Ujuzi wake wa kupika vyakula mbalimbali

**43.** Mtu anapotumia vyungo vya kawaida kupika chakula chenye utamu wa kipekee husemekana kuwa
A. ana kipawa cha upishi
B. ni mtaalamu wa kupika
C. amesomea upishi
D. ni hodari wa kupika

**44.** Mbali na kuwa mpishi Bi Aseyo pia ni
A. mshonaji
B. mwokaji
C. mwigizaji
D. mwimbaji

**45.** Bi Aseyo hupatikana katika sherehe zifuatazo zilizotajwa isipokuwa
A. sherehe za harusi
B. sherehe za mafahali
C. sherehe za kuzaliwa
D. sherehe za mahafali

**46.** Bi Aseyo aliporejea Nairobi kutoka shughuli zake sehemu mbalimbali alijisikia
A. mchangamfu
B. mwenye furaha
C. mwenye nguvu
D. mnyonge

**47.** Ili kupunguza uchovu Bi Aseyo Ba
A. Alilala ili kujipumzisha
B. Alioga maji baridi
C. Alifanya mazoezi
D. Alimeza dawa za maumivu

**48.** Bi Aseyo alipoenda kumwona daktari, daktari alimwuliza iwapo
A. alikuwa amesafiri
B. alikuwa amemeza dawa
C. amewahi kuugua malaria
D. alikuwa amemwona daktari mwingine

**49.** Baada ya matokeo ya maabara ilibainika kuwa
A. Bi Aseyo hakuwa na shida yoyote
B. Alikuwa na malaria nyingi mwilini
C. Alikuwa na malaria kidogo tu
D. alikuwa na uchovu tu

**50.** Unadhani ni kwa nini madaktari walimshughulikia sana Bi Aseyo katika aya ya mwisho?
A. Kwa sababu aliwaomba kufanya hivyo
B. Kwa sababu ni mpishi hodari
C. Kwa sababu alikuwa aende safari
D. Kwa sababu malaria ni hatari

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com